



**JARAMOGI OGINGA ODINGA UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY**  
**SCHOOL OF EDUCATION**

**UNIVERSITY EXAMINATION FOR DIPLOMA IN EDUCATION SPECIAL NEEDS**

**2<sup>ND</sup> YEAR 1<sup>ST</sup> SEMESTER EXAM 2016/2017 ACADEMIC YEAR**

**MAIN CAMPUS REGULAR**

---

**COURSE CODE: DSN 2212**

**COURSE TITLE: KISWAHILI**

**EXAM VENUE:**

**STREAM:**

**DATE:**

**EXAM SESSION**

**TIME: 2 HOURS**

---

**MAAGIZO:**

1. Swali la kwanza ni la lazima.
2. Jibu maswali mengine mawili kutoka kwa yale yaliyosalia.
3. Majibu yako yote yaandikwe katika kijitabu cha kujibia maswali ambacho utapewa.
4. Ni hatia kubeba vitabu, makala au karatasi zozote zisizorasmi katika chumba cha kufanyia mtihani.
5. Andika majibu yako kwa hati nadhifu ambazo zinasomeka kwa urahisi.
6. Kila mtahaniwa ahakikishe amemkabidhi msimamizi wa mtihani karatasi yake ya majibu.

SEHEMU A: (LAZIMA – ALAMA 30)

1. a) Eleza dhana zifuatazo:

- i) lugha (alama 3)
- ii) misimu (alama 2)
- iii) kuchanganya ndimi (alama 2)
- iv) kubadili misimbo (alama 2)
- v) utohozi (alama 2)
- vi) kiwakilishi (alama 1)

b) i) Fasihi ni nini? (alama 2)

ii) Eleza tanzu nne za fasihi simulizi (alama 4)

iii) Baada ya Mustafa kumwoa Mariamu, walifanikiwa kuzaa watoto watano: Yohana, Rebeka, Akinyi Yusufu na Musa. Rebeka aliolewa na Otieno, mtoto wa Apedor, naye Yohana akamwoa Moraa binti yake Wamalwa. Koech naye alimwoa Akinyi.

- a) Yohana anamwita Wamalwa \_\_\_\_\_
- b) Akinyi anamwita Moraa \_\_\_\_\_
- c) Watoto wa Yohana wanamwita Rebeka \_\_\_\_\_
- d) Otieno na Koech wanaitana \_\_\_\_\_
- e) Watoto wa Koech wataitana na wale wa Rebeka \_\_\_\_\_
- f) Akinyi na Musa wanaitana \_\_\_\_\_ (alama 6)

iv) Taja sayari ambayo:

- a) Ni kubwa zaidi
- b) Inakaribiana sana na jua
- c) Ni ya tatu kwa kukaribiana na jua (alama 3)

v) Taja aina mbili za magonjwa yanayosababishwa na kung'atwa na mbu (alama 2)

vi) Msimu wa mvua chache huitwa \_\_\_\_\_ (alama 1)

SEHEMU B: (CHAGUA MASWALI YOYOTE MAWILI KUTOKA SEHEMU HII - ALAMA 40)

2. a) Eleza sababu nne zilizosaidia Kiswahili kuenea nchini Kenya kabla ya uhuru (alama 8)

b) Ni jitihada zipi zimefanywa na serikali ya Kenya kukikuza Kiswahili? (alama 12)

3. a) Eleza sifa za sajili ya dini (alama 12)

b) Kwa kutoa mifano, tofautisha:

- i) Lahaja na lafudhi
- ii) kuchanganya misimbo na kubadili misimbo (alama 8)

4. a) Thibitisha kauli kwamba Kiswahili ni lugha ya Wabantu (alama 10)

- b) Ni vizuizi gani vinavyoikumba lugha ya Kihindi katika karne ya ishirini na moja? (alama 10)
5. a) Andika wingi wa sentensi zifuatazo:
- i) Mama alianua nguo yake baada ya kutoka sokoni. (alama 2)
  - ii) Mtoto alipojaribu kukata waya, umeme ulimruska chini. (alama 2)
- b) Changanua sentensi hizi kwa njia ya matawi:
- i) Yule mwanafunzi mdogo amefaulu. (alama 2)
- c) Andika katika usemi wa taarifa:
- i) Mwalimu aliwaamuru wanafunzi wote waingie darasani mara moja. (alama 2)
- d) Nyambua vitenzi hivi katika kauliya kutendesha:
- i) panda
  - ii) nywa (alama 2)
- e) Katika sentensi ifuatayo, tambua vivumishi vilivyotumika na ueleza ni vya aina gani?
- i) Niliona kile kitabu chekundu cha mwanafunzi wangu kimeraruka. (alama 4)
  - f) Eleza aina ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hizi:
    - i) Mtu yeyote anayetaka kuchukua ambacho si chake, ni mwizi. (alama 2)
  - g) Andika kinyume:
    - i) Baba alikichoma kisu ukutani kasha akakunja nguo alizoanika mchana. (alama 2)
  - g) Kanusha:
    - i) Samahani, nitakusahau. (alama 2)